# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu



2/2025

a publication of **Assemblies of Yahweh**

THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***February 2025***
***Volume LVI, Number 11***

# YALIYOMO


Page 1


**1. *Messiah katika Agano la Kale, Sehemu ya 4***
*Kuthibitisha ukweli wa Messiah kutoka kwa Agano la kale kilikuwa kitendo cha Kusanyiko la Kitume. Umeweza kufanya hivyo binafsi?*

**5 *Katika Kutafuta Masuke ya Kijani***
*Badala ya kutumia mfumo mgumu wa kuhesabu na mizunguko ya jua, Yahweh ametoa njia rahisi kuangalia kwa mwandamo wa mwezi wa masuke ya kijani wakati wa kuamua tarehe ya Pasaka*

**10 *Mwelekeo wa Kinabii: Mnyama Mkali***
*Waandishi, kama vile Elie Wiesel na wachanganuzi wengine walitoa maoni kwamba utawala wa Nazi wa Vita vya Pili vya Dunia, kwamba ulikuwa mnyama anayemeza roho.*

**17 *Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa, Sehemu ya 4***
*Mwenye-enzi Yahweh aliumba madarasa manne ya viumbe ili kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine.*


Page 5



Page 17

## Jalada Letu

*Jalada la mwezi huu linaonyesha eneo ambalo ni la kawaida kote katika Israeli-matunda mapya ya kuuzwa. Msafiri angeweza kisha kununua tunda hili, au mmiliki kumfanyia juisi safi ya kunywa.*

*Yahweh amebariki Israeli kwa matunda tele na bidhaa zingine za kilimo, kwani ni nchi nzuri ambayo inapasuka nje kwa tija ya ajabu.*

*Katika ufalme unaokuja wa Yahweh, dunia itarudi nyuma kwa hali yake ya Edeni. Unabii mmoja kama huo wa Ufalme unaokuja na wingi wake ni wa mti uliopandwa kando ya mto wa maji, unaozaa matunda yake mara kwa mara. **"Na upande huu na upande huu wa ule mto ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi: na majani ya mti huo ni ya kuponya mataifa."** (Ufunuo 22:2b).*




*Kuzaa matunda ni matokeo ya kupenda sheria za Yahweh (Zaburi 1:2-3), kuamini katika Yahweh (Yeremia 17:7-8), na kubakia katika Yahshua aliye Messiah (Yohana 15:5).*

***"Na itakuwa, kwa sababu mwazisikiliza hukumu hizi, na kuzishika na kuzitenda, basi Yahweh Elohim wako, atakutimizia agano na rehema aliyowaapia baba zako; Naye atakupenda na kukubarikia na kukuongezea, tena atau-bariki uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, nafaka zako na divai yako, na mafuta yako, maongeo ya ng'ombe zako, na wadogo wa kondoo zako, katika nchi aliyowaapia baba zako kuwa atakupa."** (Kumbukumbu la Torati 7:12-13).*

Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.

© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*



# Messiah katika Agano la Kale

Na Mzee Jacob O. Meyer

Watu wengi sana wanataka kutenganisha Agano la Kale kutoka kwa Agano Jipya. Katika kufanya hivyo, kimsingi wanaharibu mafundisho ambayo wanafunza kutoka kwa Agano Jipya. Agano la Kale linajumuisha msingi wa Imani yetu.

Katika msururu huu wa ujumbe, nimekuwa nikizingatia juu ya mada ya kupata aliye Messiah katika Maandishi ya Agano la Kale na kuthibitisha kwamba Yahshua aliye Messiah, Mwokozi na Mkombozi wetu, ametabiriwa katika Agano la Kale. Kama Yahshua aliye Messiah hangetimiza unabii huu, angeweza kukataliwa na wanafunzi wake ambao walijua Maandiko Matakatifu. Pia angeweza kukataliwa na Wayahudi wa siku Zake ambao walikuwa wakisikia

ujumbe Wake.

Yahshua aliye Messiah kweli alitimiza unabii kumhusu Yeye katika Agano la Kale. Manabii wa Agano la Kale walifanya utabiri kuhusu Messiah atakayekuja, na Messiah huyu alikuwa awe Mfalme aliyetiwa mafuta wa Yahweh. Atakuwa mtawala wa ufalme wa Mbinguni wakati utaanzishwa duniani humu kuanza utawala wa Milenia.

Kote katika Agano la Kale, Yahshua aliye Messiah ni mtu wa kati. Basi na tuchukue mtazamo wa karibu wa Maandiko hayo ambayo yanao unabii ambao ulifanywa miaka mamia, na hata maelfu, kabla ya kuzaliwa Kwake. Katika Yeremia mlango wa 23, kuanzia katika mstari wa 5, tunasoma, ***"Tazama siku zinakuja, asema Yahweh, nitakapomchipushia Daudi Chipukizi la haki; naye atamiliki kama mfalme na kutenda kwa hekima, naye atafanya hukumu na haki katika nchi."***

Hapa tunapata unabii wa Mwana mkuu wa Daudi. Mjukuu wa Daudi anarejelea kwa Tawi ambalo lingekuwa linatoka kwa ukoo na familia yake ambalo hatimaye lingetawala juu ya dunia hii. Angekuwa Mfalme aliyetiwa mafuta, aliyetabiriwa kutawala na kufanikiwa, kutekeleza hukumu na haki kote duniani.

Gundua Yeremia 23:6 ***"Katika siku zake Yuda ataokolewa, na Israeli atakaa salama, na jina lake atakaloitwa ni hili, Yahweh ni haki yetu*[Yah Zidkenu]*."*** Tunapochambua mstari wa 6, lazima tugundue kwamba Israeli anakaa kwa usalama, akiwa amerejea tena kwa ardhi yao, na wakati Yuda atakuwa ameokolewa, basi hakuna tena hitaji yoyote ya Mwokozi. Jina *Yahshua aliye Messiah* linamaanisha *Yahweh ni wokovu*. Jina lake lilitolewa kote katika Agano la Kale: "*wokovu wangu*, anasema Yahweh," au "Yahshua wangu." Zaidi ya hapo zingatia Yeremia 23:7-8. Kwa wazi, tunaweza kutambua marejesho ya Israeli kwa nchi yao, kama tunavyoweza kuona kwa kulinganisha Luka 1:68-75.

Katika Mathayo 1:21, tunasoma kwamba malaika wa Yahweh anampa Mwokozi Jina lake kabla ya kuzaliwa Kwake. Alikuja kwa Yusufu na kutangaza Jina la mwana wa Yahweh ambaye angezaliwa na bibi yake Mariamu (wakati mwingine akiitwa Mary). Jina lake lilitolewa kwa njia isiyo ya kawaida, mmoja wa watu wachache tu ambao walipewa majina kabla ya kuzaliwa kwao.

Tunapata katika Maandiko Matakatifu kwamba watu wachache hivyo kweli waliitwa; mmoja wa hao walioitwa alikuwa Koreshi, pia akiitwa messiah (mfalme aliyetiwa mafuta). Alikuwa mtawala wa Uajemi ambaye alishinda Babeli. Kisha aliwakomboa Yuda na kuwatuma warudi Nchi Takatifu katika siku za Nehemia na Ezra.

Yahshua aliye Messiah, kisha, alikuwa utimilifu wa aina ya Koreshi, aliye Messiah, mmoja ambaye angefungua Yuda katika terehe fulani ijayo. Angemwokoa Yuda; sio Yuda pekee, lakini, pia Israeli. Angewaleta tena makabila kumi na mawili ya Israeli katika Nchi Takatifu, nchi ya mababu zao ambapo Ufalme utaanzishwa na itakuwa eneo la makao makuu ya Ufalme wa Kimessiah duniani. Utawala wa milenia utaanzishwa Yerusalemu na kutoka hapo utaenea kwa miisho ya dunia.

Ni wapi kwingine kuonekana kwa Yahshua aliye Messiah kumetabiriwa katika Maandishi ya Agano la Kale? Kama tutageukia kwa Mika mlango wa 5, tunapata hapo unabii muhimu sana. Ni unabii mkubwa kwa sababu unatuambia kwa maelezo ni wapi Yahshua aliye Messiah angezaliwa. Pia unaelezea kwetu mambo mengi makuu kumhusu Yeye.

Unaweza kukumbuka wakati mamajusi walikuja kutoa heshima kwa Yahshua aliye Messiah baada ya kuona nyota yake mashariki? **"Yahshua alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi katika siku za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashiriki walifika Yerusalemu, wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?"**(Mathayo 2:1-2). Katika ukweli, hili lilikuwa tusi kwa Herode. Herode alikuwa mfalme wa Wayahudi na alikuwa akitafuta kuendeleza nasaba yake. Kwa busara akawaita ndani wenye busara wa taifa lake na kuwauliza ni wapi Messiah alipaswa kuzaliwa, na wenye busara wakamjibu kwamba alipaswa kuzaliwa katika Bethlehemu nchi ya Yuda. Iliandikwa katika manabii, walielezea. Herode akawatuma mamajusi(magi), na wakaenda Bethlehemu, hadi mahali ambapo nyota iliwaelekeza wao.

Mamajusi hao walikutana na Yahshua aliye Messiah kama mtoto mchanga, sio anayekaa katika banda, lakini katika nyumba. Yusufu na Miriamu walikuwa wamepata nyumba ya kutosha kwao wenyewe. Miriamu, mamake Yahshua alikuwa wa ukoo wa familia ya Daudi, kama alivyokuwa Yusufu, ingawa hakuwa baba Yake wa kweli, lakini alidhaniwa kama baba (baba wa kambo) wa Yahshua. Angalia Luka 3:23. Baba ya Yahshua aliye Messiah alikuwa Roho Mtakatifu wa Yahweh ambaye alizalisha Mwana Wake kama binadamu wa kidunia kupitia bikira Miriamu.

Ruhusu tuchukue kwenye mazingatio baadhi ya Maandishi haya. Kwanza kabisa tutageukia kwa Mika mlango wa 5, na tutaanza kusoma kwa mstari wa 2, ***"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni***



***Mfalme Daudi alilelewa karibu na mji mdogo wa Bethlehemu. Daudi alichunga kondoo katika ujirani wa Bethlehemu. Katika Bethlehemu, nchi ya Yuda ilikuwa nyumbani kwa familia ya Yese. Kungekuja fimbo kutoka kwa Yese na chipukizi kutoka kwa mizizi yake kulingana na unabii wa Isaya 11:1-11. Huu ulikuwa unabii wa Yahshua aliye Messiah, kwa sababu Daudi tayari alikuwa amekufa wakati huo unabii ulikuwa unasemwa na kuandikwa. Haungetumika kwa Daudi, lakini kwa uzao wake***

***mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele."***

Basi tuchambue mstari huo kwa uangalifu. Mfalme Daudi alilelewa karibu na mji mdogo wa Bethlehemu. Daudi alichunga kondoo katika ujirani wa Bethlehemu. Katika Bethlehemu, nchi ya Yuda ilikuwa nyumbani kwa familia ya Yese. Kungekuja fimbo kutoka kwa Yese na chipukizi kutoka kwa mizizi yake, kulingana na unabii wa Isaya 11:1-11. Huu ulikuwa unabii wa Yahshua aliye Messiah, kwa sababu Daudi tayari alikuwa amekufa wakati huo unabii ulikuwa unasemwa na kuandikwa. Haungetumika kwa Daudi, lakini kwa watoto wake.

Unabii huu wa kimessiah katika Agano la Kale haungetumika kwa Hezekia, kulingana kwa njia ambayo baadhi ya marabi walitazama vifungu hivyo, kwani katika Maandiko, unabii katika Isaya 9:7 unasoma, ***"Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe…."*** Bado utawala wa Hezekia ulimalizika na amani haikuanzishwa. Katika utawala wa Yahshua aliye Messiah, hakutakuwa na mwisho wa maongeo ya serikali yake ya Haki, au ya amani kote duniani, kwa sababu atatawala dunia hii kwa haki na uadilifu milele.

*Bethlehemu*, katika Kiebrania ina maana ya *nyumba ya mkate*.Bethlehemu ilikuwa katika eneo la ukulima lenye rutuba, mahali ambapo chakula kingepatikana, na Yahshua aliye Messiah angewalisha watu wake kama mchungaji. Atawalisha kundi lake kama mchungaji mwenye haki. Neno *Efrata*, katika Kiebrania, lina maana ya *yenye matunda*. Unapokumbuka kwamba, nyuma katika Mwanzo, Mzee Yakobo pamoja na msafara wake mkubwa

na familia yake kubwa, ng'ombe na kondoo, walikuja Bethlehemu. Ilikuwa karibu na Bethlehemu ambapo Raheli alianza utungu wa kuzaa mtoto. Kama anakaribia pumzi yake ya mwisho katika uchungu, akiwa ametoa maisha yake kumzaa mwana wake Benyamini, alikufa na akazikwa Bethlehemu, Efrata. Ilikuwa hapa basi ambapo *Benyamini* (jina linamaanisha *mwana wa mkono wangu wa kuume*, katika Kiebrania) alikuwa na mahali pake pa kuzaliwa.

Basi tuzingatie kidogo zaidi kwa karibu Mika 5:2, sasa kwamba tumeweka jukwaa tayari. ***"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo***[sana][kuhesabiwa] ***miongoni mwa maelfu ya Yuda...."***Neno *maelfu* katikaKiebrania ni *'elepheem* na linamaana ya *kikosi kilichohesabiwa, ambao wameweza kuhesabiwa kupitia sensa, au idadi 1,000*. ***"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo*** [kuhesabiwa]***miongoni mwa maelfu ya Yuda, kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli...."***Mfalme wa Israeli angekuja kutoka Bethlehemu; angezaliwa katika Bethlehem, kama alivyokuwa Daudi aliye Mfalme, babu yake.

Fahamu kwamba unabii huu ulisemwa na Mika, na alitabiri kabla ya wakati ambao makabila ya Israeli yalienda kwenye utumwa. Alitabiri miaka mia kadhaa baada ya utawala wa Daudi. Ilikuwa Daudi ambaye aliimarisha makabila kumi na mawili ya Waisraeli kwenye ufalme,mfalme ambaye alianzisha ufalme mkubwa wa Israeli ambao hatimaye ulipitishwa mikononi mwa mwanawe Suleimani.

Kwa hivyo, Mika hangekuwa anatabiri kuhusu Mfalme Daudi, mwenyewe, lakini Mwana wa Daudi, Mjukuu wake mkuu, mmoja ambaye alipangwa kutawala Israeli mpaka apeleke Ufalme kwa baba Yake Yahweh. Mtu huyu binafsi anaelezewa: ***"Ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele."*** Alikuwepo kabla ya kuzaliwa kwake kwa kibinadamu. Alikuwa *logos*, kama Mtume Yohana anavyosema katika mlango wa kwanza wa kitabu chake. Alikuwa *logos*, Neno, Msemaji, ambaye alikutana na, na kuwa na mawasiliano na, wazee wa zamani na Israeli, wakati, Baba wa Mbinguni kamwe hakuonekana wala kusikika. Angalia Yohana 1:18 na 5:37.

Unabii unaendelea ***"Kwa sababu hiyo atawatoa, hata wakati wa kuzaa kwake aliye na utungu: ndipo hayo mabaki ya nduguze watawarudia wana wa Israeli."*** Ingekuwa katika wakati wa kurudi kutoka kwa utumwa ambapo Messiah angefanya kuonekana Kwake, na siku hiyo sasa imekaribia. Itakuja hivi karibuni!

Tuzingatie basi wazo linalopatikana katika Mwanzo 49:10. ***"Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, wala fimbo ya mtawala kati ya miguu yake, hadi Shiloh aje; ambaye kwake utakuwa utiifu wa watu wake."*** Yahshua aliye Messiah ni Mfalme wa Amani ambaye atakuja kuanzisha ufalme wa amani duniani humu. Atatawala mataifa na kuanzisha haki na amani milele. Utakuwa na sehemu katika zama hizo za Ufalme? SNB




## Swali:

Chapisho na mtumishi wa redio, lenye tarehe ya Aprili 6, 1976, lilisema kwamba katika Israeli "mavuno ya nafaka iliyoiva zaidi hayataanza mpaka nafaka iwe ngumu na unyevu kuwa umeshuka kwa asilimia 11-12." Dondoo zaidi ya nakala sawa kutoka kwa barua yake inasoma, "… katika Yeriko, ngano na shayiri hazionyeshi rangi ila kijani na, masuke, kama yaliyotarajiwa yalikuwa katika hatua ya maziwa-maziwa bila ubaguzi…" ikiwa, kama ulivyoonyesha, mimea lazima iwe iliyoiva vya kutosha kwa mavuno-ambayo inaonekana sahihi- na haikuwa iliyoiva kwa sikukuu mwaka huu, basi kalenda yetu ni wazi ni mbali na mwezi mmoja. Utatoa maoni kwa hali hii ya kushangaza?



*The author in Israel, 2007*

# Kutafuta Masuke ya Kijani

## Jibu:

Nikiwa nimepokea barua kadhaa kupitia kwa barua kutoka kwa wateja mbalimbali wa **The Sacred Name Broadcaster** pamoja na maswali mengi kupitia kwa miaka kuhusiana na kalenda ya kimaandiko, tungependa kweli kutoa maoni. Walakini, ruhusu kwanza tuchukue maoni hayo moja kwa moja kutoka kwa Biblia.

Kwanza kabisa, mavuno **yote** ya nchi HAYAHITAJIKI kuwa yaliyoiva wakati mwezi wa kwanza wa mwaka unawasili, ambapo tunatunza siku takatifu za Yahweh za msimu wa machipuko. Lazima tutunze siku takatifu ambazo Yahweh ameanzisha na katika wakati sawa wa mwaka alipozianzisha.

Tambua Kumbukumbu la Torati 16:5-6 ukiyapa uzingatiaji maalum maneno yaliyotiliwa mkazo. ***"Usimchinjie pasaka ndani ya malango yako yote akupayo Yahweh, Elohim wako; ila mahali atakapochagua Yahweh, Elohim wako, apakalishe jina lake, ndipo mtakapomchinjia pasaka jioni, katika machweo ya jua, KATIKA MSIMU KAMA ULIOTOKA MISRI."***

Kujua lini tutaweka Pasaka, lazima tutambue msimu wake sahihi. Tunaweza kwa usahihi kutambua msimu wa mwaka wakati Israeli alitoka Misri? Geuki kwa Kutoka 9:31-32. ***"Kitani na shayiri zilipigwa; maana shayiri zilikuwa na masuke na kitani zilikuwa katika kutoa maua. Lakini ngano na kusemethu hazikupigwa; maana, zilikuwa hazijakua bado."***

Sehemu hii ya simulizi la Kutoka linaashiria kwa wakati ambapo pigo la mvua ya mawe liliharibu nchi ya Misri. Pigo la mvua ya mawe lilikuwa pigo la nane, na lilitokea kabla tu ya kuanza kwa mwezi wa kwanza wa kimaandiko. Pengine siku saba kabla ya mwaka mpya wa kimaandiko, kwani mapigo ya nzige na giza yalitokea kabla ya mwaka mpya. Tafadhali angalia Kutoka 10. Mwaka mpya wa kimaandiko mara moja unafuata pigo la giza.

Mwenye-nguvu Yahweh anaita mwezi wa kwanza wa mwaka *Abib*, maana yake *masuke ya kijani*, au *vichwa vipya vya shayiri* kama tulivyoona tayari katika Kutoka 9:31. Neno katika **Strong's Concordance Hebrew Dictionary** limeorodheshwa kama #24, "*kutoka kwa mzizi usiotumika (kumaanisha kuwa laini); kijani, hiyo ni, masuke machanga ya nafaka; kwa hivyo jina la mwezi Abib au Nisan.*" Wakati ni ambao hilali ya kwanza dhaifu ya mwezi ambayo inaonekana katika anga ya jioni kama mwezi mpya unaanza kujenga upya katika mwanga. Angalia **Strong's Exhaustive Concordance** #2318 na # 2320. Mwezi huu mpya lazima uwe ni wa kwanza kuonekana kwenye anga ya jioni wakati kunayo MASUKE YA KIJANI YALIYOKUA KAMILI YA SHAYIRI yanayoonekana mashambani. Sasa tafadhali baini kwamba chapisho lililonukuliwa katika mwanzo lilionyesha kwamba kulikuwa kwa kweli na **masuke ya shayiri mwaka huo katika Aprili 6 katika kila mahali ambapo mwandishi alitembea katika Israeli.**

Kwa sababu hiyo, mwezi ambao ulianza Aprili 1, 1976, ambao ulikuwa siku ya kwanza ya kimaandiko ya mwaka mpya, ulikuwa kweli mwezi wa masuke ya kijani, na Pasaka ilitunzwa sahihi mwaka huo na Assemblies of Yahweh. Hali sawa iliendelezwa tena katika 1984, wakati makundi fulani ya kidini yalitunza Ukumbusho mapema (katika Machi), wakati Assemblies of Yahweh

ilitunza Pasaka na Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu katika Aprili. Tena, katika 1986, makundi mengi yalifuata tarehe iliyowekwa ya Ukristo ya Easter ya Machi wakati Assemblies of Yahweh walitunza Ukumbusho katika Aprili. Karibu kila mwaka, tangu 1984, mwakilishi wa Assemblies of Yahweh amesafiri Israeli kukagua maendeleo ya mavuno ya shayiri kuhakikisha binafsi usahihi wa msimu.

Katika wakati huu, inakuwa muhimu kwamba tufafanue kabisa neno *Abib*. Ikiwa tunaweza kuamua maana ya neno, kusoma kwetu kwa mada hii kutachukua mtazamo sahihi, na tutuweza kuelekezwa kwa msingi imara wa mafundisho safi. Nukuu zifuatazo zimechukuliwa kutoka kwa kazi za utafiti na zimeandikwa na wasomi mashuhuri wa Kibiblia na lugha ya Kiebrania. Basi tuone nini zinasema kuhusu maana ya neno Abib.

"*Abib, kuchipua chipukizi. Mwezi wa kwanza wa mwaka takatifu na wa saba wa kiraia wa Waebrania, katika ya 15 ambayo Israeli aliondoka Misri. Inaanza katika Mwandamo wa mwezi wa Aprili au Machi (kulingana kwa Marabi) na ulianzishwa mwezi wa kwanza katika kumbukumbu ya kukombolewa kutoka utumwa wa Kimisri.*" (**Young Analytical Concordance**).

"*Abib (kutoka kwa mzizi Avav), m.,masuke ya nafaka, masuke ya kijani, Law. 2:14, Kut. 19:31, hodes haaviv 'mwezi wa masuke ya kijani,' kwa kipindi cha baadaye ukiitwa Nisan, kuanzia kwa mwandamo wa mwezi wa Aprili (au Machi, kulingana kwa marabi), mwezi wa kwanza wa mwaka mzee [kama ilivyowekwa katika kutoka kwa Misri], Kut. 13:4, 23:15; Kumb. 16:1*" (**Tregelles' Gesenius Chaldee Lexicon of the Old Testament**).

"*Abib- 1.Masuke (ya nafaka) yaliyokomaa lakini bado laini, nafaka ambayo ilikuliwa labda kusuguliwa au kuchomwa, Law. 2:14- 2. (mwezi wa masuke), Machi/Aprili; baadae Nisan; Kut. 13:4.*" (**A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament Holladay**).

"*Abib (masuke ya nafaka): Jina la mwezi wa kwanza wa mwaka wa Kebrania (Kut. 12:2; linganisha 13:4), ya kulingana kwa mwezi wa Kibabeli wa Kiebrania wa baada ya uhamisho Nisan.*" (**Jewish Enclopedia**, Juzuu 1).

"*Abib (kutoka kwa mzizi wa kizamani avav, kuzaa matunda), vizuri, kichwa cha au masuke ya nafaka (Law. 2:14, 'masuke ya kijani; Kut. 13:31, 'masuke') kwa hivyo mwezi wa nafaka mpya iliyokomaa (Kut. 13:4, 23:15, 34:18; Kum. 16:1) mwezi wa kwanza wa mwaka wa kikanisa wa Wayahudi, baadaye (Nehe. 2:1) ukiitwa Nisan… kwa wakati ambao nafaka ya kwanza ilikomaa katika Palestina.*" (ya **McClintock and Strong's, Cyclopedia of Biblical, Theological, and Ecclesiastical Literature**).

"*Abib, masuke machanga ya shayiri au nafaka nyingine.*" **(International Standard Bible Encyclopedia).**

**"***Mwezi ambao tangu sasa ulikuwa uwe wa kwanza wa mwaka, na mara nyingi umeonyeshwa hivyo unaitwa Abib (mwezi wa masuke) katika Kut. 13:4, 23:15, 34:18; Kum. 16:1, kwa sababu nafaka ilikuwa basi katika masuke; baada ya utumwa uliitwa Nisan (Neh. 2:1, Esta 3:7). Inalingana karibu sana kwa Aprili yetu.*" (**Keil and Delitzsch Commentary of the Old Testament**, Juzuu 1).

Kunaweza kuwa na shaka kidogo kutoka kwa kusoma marejeleo haya (ambayo yote yanakubaliana) kwamba mwezi wa Abib ni wakati ambapo **shayiri iko katika masuke au kichwa**. Nafaka kwenye vichwa imekua kabisa, lakini bado katika hatua ya unga, kwani lazima iwe imekomaa kutoa sadaka inayohitajika ya mganda wa kutikiswa. Mwezi unaanza wakati vichwa vinavyokua bado ni kijani, kwani, ndani ya mwezi huo, nafaka itakomaa inavyotosha ili kwamba baadhi yazo zinaweza kuliwa kwa kuchomwa juu ya moto. Baadhi ya nafaka, wakati zinakaushwa bandia juu ya moto zinaweza kutumiwa kufanya unga na mkate. Ni tamko la ulimwengu kote la wasomi wote walionukuliwa hapo juu kwamba mwezi huu unalingana kwa miezi ya Kirumi ya Machi- Aprili. Lazima tukumbuke kwamba nafaka haihitaji kuwa zimeiva wakati mwezi unaanza, *lakini lazima ziwe nafaka zilizokua kikamilifu katika vichwa vya kijani*.

**Mwezi wa Abib** unamaanisha mwezi ambao masuke ya kijani ya nafaka yanakomaa. Kama mwezi unaendelea, mchakato wa kukomaa unaendelea hivyo kwamba nafaka za kwanza haswa (ingawa pengine bado laini) zingeweza kuletwa kwa Hekalu la Yahweh, kupepetwa, na kutolewa kama mganda wa kutikiswa. Sadaka hii ilifanywa wakati wa Sikukuu za mkate usiotiwa chachu. Baadhi ya nafaka kisha zilipigwa (kama galoni ilihitajikana kukaushwa kwa kuchomwa juu ya moto wazi. Ilichukuliwa, inapokauka, na kusagwa kwenye unga, ambayo sehemu ilitolewa juu ya madhabahu kwa Yahweh. Hii ilikuwa ibada chini ya mfumo wasadaka, na ni muundo muhimu kwa Waabudu wa Kweli kufuata kuweka tarehe Pasaka na kuelewa maana yake katika maana ya kiroho katika Agano Jipya. Hatua ya unga ya vichwa vya shayiri lazima ingefikiwa katika wakati wa mwandamo wa mwezi, hivyo baadhi ya nafaka zingepigwa nje na kukaushwa

kwa kuchomwa kufanya unga wa kwanza kwa mkate mpya.

Tunaweza basi kuthibitisha ukweli huu kwa ukamilifu. Geuka namikwa Walawi 23, na tutasoma mistari ya 9-16. Tafadhali baini haswa vifungu ambavyo vimesisitizwa. ***"Kisha Yahweh akanena na Musa na kumwambia, Nena na wana wa Israeli, uwaambie, Hapo mtakapokuwa mmekwisha kuingia hiyo nchi niwapayo, na kuyavuna mavuno yake, ndipo mtakapomletea kuhani mganda wa malimbuko ya mavuno yenu; naye atautikisa mganda mbele za Yahweh, ili kwamba ukubaliwe kwa ajilli yenu; siku ya baada ya Sabato kuhani atautikisa. Na siku hiyo mtakayoutikisa mganda, mtasongeza mwana-kondoo wa kiume mkamilifu wa mwaka wa kwanza awe sadaka ya kuteketezwa kwa Yahweh. Na sadaka yake ya unga itakuwa sehemu za kumi mbili za efa za unga mwembamba uliochanganywa na mafuta, ni kafara iliyosongezwa kwa Yahweh kwa moto kuwa harufu ya kupendeza; na sadaka yake ya kinywaji itakuwa ni divai, robo ya hini. Nanyi msile mkate, wala NAFAKA ILIYOCHOMWA, wala MASUKE MACHANGA, hata siku iyo hiyo, hata mtakapokuwa mmekwisha kuleta sadaka ya Elohim wenu; hii ni amri ya milele katika vizazi vyenu katika makao yenu yote.***

***"Nanyi mtajihesabia tangu siku ya baada ya Sabato, tangu siku hiyo baada ya sabato, tangu siku hiyo mlipouleta mganda wa sadaka ya kutikiswa; zitatimia Sabato saba; hata siku ya pili ya hiyo sabato ya saba mtahesabu siku hamsini, nanyi mtamsongezea Yahweh sadaka ya unga mpya."***



Sasa, ruhusu tutambue kifungu kingine bado ambacho ni sambamba na ambacho kimenukuliwa tu. Hiki kinapatika katika Kutoka 23:19. Tena, baini maneno yaliyosisitizwa. ***"Ya kwanza ya malimbuko ya nchi yako utayaleta na kuyatia ndani ya nyumba ya Yahweh Elohim wako."*** Mstari huu sawa unaofanana unarudiwa katika Kutoka 34:26. Kwa sababu hiyo, hapa tunayo maagizo kwamba **mganda wa KWANZA haswa wa nafaka uliovunwa** utaletwa kwa Hekalu la Yahweh na kutolewa kama sadaka maalum ya mganda wa kutikiswa. Sherehe hii ilifanywa katika hekalu wakati wa Sikukuu ya Mkate usiotiwa Chachu.

**Mganda wa kutikiswa ulikuwa sadaka ambayo iliwakilisha ufufuo wa** Yahshua aliye Messiah. Yahshua Mwenyewe alimalizia sadaka hii kwa ufufuo wake wakati Miriamu Magdalene alimtambua vibaya kuwa Yeye ni mtunza bustani, Yohana 20:15. Yahshua alikuwa inavyoonekana, binafsi amekata mganda wa mwisho uliokubalika chini ya mfumo wa sadaka na alikuwa anauchukua kuutoa katika hekalu ya Yahweh kwenye safari Yake kujiwasilisha Mwenyewe Mbinguni mbele ya Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wa Mbinguni.

Kwa sababu hiyo, sadaka hii ya mganda wa kutikiswa lazima iwe **nafaka ya KWANZA kabisa ambayo imeiva vya kutosha kukatwa na kupigwa nje. Ni** ***mganda mmoja*** tu unaohitajika kwa sadaka. Nafaka zingine zinaweza kubakia katika hatua mbalimbali za kukomaa, kijani, maziwa-maziwa au unga. Mahitaji ya pekee ni kwamba kuwe na **mganda MMOJA uliokomaa wa nafaka.**

Mstari mwingine wa Maandiko unabeba kwa uzito juu ya mada hii, na huo ni ambao unapatikana katika Kumbukumbu la Torati 16:9. ***"Jihesabie majuma saba; Anzia kuhesabu majuma saba kutoka wakati uanzao kutia mundu katika mmea*** [nafaka] ***uliosimama.***(***New English Bible***)***"***

Nafaka iliyosimama ni hiyo ambayo bado haijavunwa. Sasa kumbuka, tayari tumeona kwamba **ya KWANZA ya malimbuko** (**mganda wa kwanza hasa**) lazima uletwe kwa nyumba ya Yahweh; na hivyo, hesabu ilianza kuelekea Pentekoste, au Sikukuu ya Majuma. Katika wakati ambao mganda huu wa kutikiswa unatolewa, kunaweza bado kuwa na nafaka katika hatua mbalimbali za kukomaa, lakini hiyo yote muhimu ni kuweka mundu kwa viganja vya kwanza vya nafaka iliyokomaa kufanya mganda na kuileta kwa Hekelu la Yahweh.

Mwenye-nguvu Yahweh hajakusudia kutuchanganya sisi kuhusiana na jinsi anataka sisi kuonyesha mwezi wa kwanza wa kimaandiko wa mwaka. Lazima ubainishwe na hilali ya kwanza ya mwezi wakati kunayo **masuke kamili,YA KIJANI ya nafaka** (shayiri) shambani. Basi tugeukie kwa Walawi 2:14:16. ***"Nawe kwamba wamtolea Yahweh sadaka ya unga ya MALIMBUKO, utatoa hiyo nafaka katika MASUKE YAKE ILIYOCHOMWA MOTONI, nafaka ILIYOPONDWA YA MASUKE MABICHI, NDIYO UTAKAYOLETA KUWA SADAKA YA UNGA YA MALIMBUKO YAKO. Nawe utatia mafuta juu yake, na kuweka ubani juu yake; ni sadaka ya unga. Huyo kuhani atautekeza ukumbusho wake, yaani, sehemu ya nafaka iliyopondwa ya hiyo sadaka, na sehemu ya mafuta yake, pamoja na ule ubani wake wote; ni kafara ya kusongezwa kwa Yahweh kwa njia ya moto."***

Unatambua yale umeweza tu kusoma? Tafadhali soma juu ya kifungu hiki tena, na kubaini maneno yaliyosisitizwa kwa makini. Sadaka ya malimbuko ilitolewa kwa Yahweh **hata ingawa nafaka inaweza kuwa haijaiva kabisa.** Kama nafaka ziko katika hatua ya unga ya baadae, zinaweza kukaushwa kwa kuchomwa. Nafaka maziwa-maziwa haziwezi kukaushwa au kuchomwa.Umetambua marejeleo kwa kuchomwa katika Maandiko yote hapo juu ambayo yanatoa **maagizo wazi** jinsi ya kutoa **sadaka ya MALIMBUKO**?



Ugunduzi wa kutia msukumo uliofanywa na mhariri idadi ya miaka iliyopita katika jumba la makumbusho la Israeli katika Yerusalemu ulikuwa onyesho la ***shayiri ilichomwa*** ambayo ilikuwa imegunduliwa katika uchimbuaji wa akiolojia katika ***Gilgali***. Inavyoonekana, utiifu wa mabaki ya Waisraeli kwa Sheria ya Yahweh uko katika maonyesho kuwatia moyo wote ambao wanatamani kuwa katika maelewano na Agano Lake la Torati.

Mahitaji ya mganda wa kutikiswa wa malimbuko ni kuchukua **konzi za KWANZA za nafaka iliyoiva** na kuzikata kwa sadaka kwa Yahweh. Mganda wa kwanza kisha ulikuwa uletwe Hekaluni mwa Yahweh na kupigwa nje, hata ingawa nafaka zinaweza kuwa bado hazijafikia asilimia 11-12 ya hatua ya unyevu kwa uvunaji wa kisasa wa mitambo. Nafaka ingekaushwa kwa wakati ikichomwa juu ya moto, kwani ilikuwa katika hatua ya unga na haingezorota wakati inachomwa (kama vile ingefanya katika hatua ya maziwa-maziwa), na, wakati imekauka vya kutosha, ilisagwa kwenye unga. Kisa ilipepetwa kupitia ungo 13 mpaka ikakuwa laini kabisa.konzi za kwanza chache za unga kisha zilitolewa juu ya madhabahu. Baada ya sadaka hii ya malimbuko imetolewa kwa Yahweh katika shukrani kwa mavuno yanayokuja, watu wa nchi wangeanza kula masuke ya kijani (ndio, umetambua kwamba kulikuwa bado **masuke ya kijani ya nafaka** katika shamba wakati mganda wa kwanza kuiva ulitolewa!), nafaka iliyochomwa, au mkate uliofanywa kutoka kwa mavuno mapya.

Wazi namna gani na rahisi ni maagizo kutoka kwa Yahweh katika Neno Lake wakati tunayachunguza kwa uangalifu. Tusome basi kifungu kingine na kukichambua kwa uangalifu tu. Hiki kinapatikana katika Yahshua 5:10-12. ***"Basi wana wa Israeli wakapanga hema zao huko Gilgali; nao wakatunza Pasaka katika tambarare za Yeriko, siku ya kumi na nne ya mwezi, jioni. Nao wakala katika mazao ya nchi siku iliyoandama hiyo sikukuu ya pasaka, mikate isiyotiwa chachu naNAFAKA ILIYOCHOMWA, ya mazao ya nchi siku iyo hiyo, ndipo mana ikakoma siku hiyo. Wana wa Israeli hawakupokea mana tena; na mwaka huo wakala vilivyomea katika nchi ya Kanani mwaka huo."*** (***New English Bible***).

Mara moja zaidi, tunaweza kuona kwamba Waisraeli hasa walifuata maagizo ya Walawi 2:14-16. Walikula mikate isiyotiwa chachu na**nafaka zilizochomwa** zilizofanywa kwa mazao ya nchi ile. Pasaka ya kwanza Kanani ilifanyika katika nyanda za chini za tambarare ya Yeriko. (**Kutoka kwa mahali hapa hasa** kwa kambi ya Waisraeli katika **Gilgali** wanaakiolojia walileta onyesho la shayiri iliyokaushwa ambayo iliwekwa kwa maonyesho katika jumba la maonyesho la Israeli.)

Sasa ruhusu tumkumbushe kila msomaji kwa ukweli ambao hauwezi kupuuzwa. Barua iliyonukuliwa hapo juu **inakubali** kwamba kulikuwa na masuke ya kijani, au vichwa, vya shayiri katika tambarare za Yeriko. Mwandishi anakubaliana na hilo! Barua inayo tarehe ya Aprili 6, ambayo inamaanisha kwamba lazima alikuwa ameona vichwa vya kijani vya shayiri hapo siku kadhaa mapema, ikiwezekana katika Aprili 1 hadi 4 (kutokana na urefu wa safari ya kurudi nyumbani). Mganda wa kutikiswa katika 1976 ungeweza kukatwa katika Aprili 18, **ambao ni WIKI MBILI KAMILI baadaye.** Nikiwa nimekuzwa shambani mwenyewe, ninajua kwamba vichwa vya nafaka vinaweza kukua mbali ya kutosha katika wiki mbili kwamba hatua ya unga inaweza kufikiwa kwa urahisi, hasa katika shayiri, kwani shayiri ni mazao inayokomaa haraka.Kula nafaka iliyokaushwa, au hata kusaga unga fulani kutoka kwa ya kwanza ya nafaka inayokomaa ingewezekana kwa kweli.

Lakini ruhusu niashirie kwamba mavuno yote ya shayiri hayahitaji kuwa tayari kwa kukatwa wakati mganda wa malimbuko ulitolewa kwa Yahweh na baadhi ya MASUKE YA KIJANI yaliyochomwa kwa ajili yakuliwa. Mavuno yalifuata baadaye, na kulikuwa na wiki saba kukusanya ndani mavuno ya nafaka mpaka malimbuko ya mavuno ya ngano ambayo yalitolewa katika siku ya Shavuoth (Pentekoste), Kutoka 34:22. Wakati Waisraeli walikuwa wanatunza Sikukuu za Mikate Isiyotiwa Chachu katika Yerusalemu, mganda wa kwanza uliokomaa wa shayiri ulitolewa kama mazao ya kwanza kwa Yahweh katika Hekalu. Kufuatia Sikukuu, Waisraeli walirudi nyumbani na wangeweza kuanza mavuno yao wenyewe ya shayiri, ambayo ilikuwa iliyoiva kabisa wakati huo.

Msimu wa kilimo katika Nchi takatifu unaonyesha mavuno ya kiroho ya binadamu ya dunia. Ya kwanza ya malimbuko kuvunwa yalikuwa Yahshua aliye Messiah. Kisha wakafuata watu Wake wa Kusanyiko la Kitume, sasa wakiwa wamelala kaburini wakisubiri ufufuo katika mwisho wa wakati. Malimbuko ya mavuno ya ngano-mavuno makubwa-karibuni yatakusanywa, na watu hata sasa wako katika mchakato wa kukua. Mavuno ya mizabibu pia yanakua.

Ngano na zabibu zitavunwa, karibu tu kwa wakati mmoja, katika mwisho wa wakati. Ngano itakusanywa kwanza; hili linawakilisha watu wenye haki ambao wanamwabudu Yahweh katika Yahshua na wametimiza kwa uaminifu masharti ya Agano Lake. Zabibu zitakusanywa (hizi zinawakilisha watu waovu wa dunia) kutupwa kwenye shinikizo kubwa la divai la ukali wa ghadhabu za hukumu ya Yahweh, Ufunuo 14:14-20.

Sasa basi tuchukue kwenye mazingatio ushahidi fulani wa kihistoria ambao tumeweza kuja kwa ufahamu sahihi wa msimu wa mavuno wa Palestina. Nukuu ifuatayo ni kutoka kwa kitabu, **The Temple, Its Ministry and Services as they were at the Time of [Yahshua] Messiah**, kilichoandikwa na Dr. Alfred Edersheim. Kopi katika umilikaji wetu ilichapishwa na Ira Bradley & Company, Boston, 1881.

**"***Kila wakati ikijibiwa kwa uthibitisho, walikata shayiri kwa kiasi cha efa au omeri kumi, au seah tatu, ambazo ni sawa kwa kama peksi tatu na pinti tatu za kipimo cha kiingereza. Masuke yaliletwa kwenye Ua wa Hekalu, na kupigwa kwa fimbo au mabua, ili kwamba wasiumize nafaka; kisha 'wakachoma' juu ya sufuria iliyotobolewa mashimo ili kwamba kila nafaka ingeweza kuguswa na moto, na mwishowe kufunuliwa kwa upepo. Nafaka iliyotayarishwa hivyo ilisagwa katika kinu cha shayiri, ambacho kiliacha maganda yakiwa mazima.kulingana na wengine, unga ulipitishwa mfululizo kupitia ungo kumi na tatu, kila moja ya karibu kuliko*

*Continued on page 21.*



# Mnyama Mkali

Tumekuwa tukijifunza alama ya mnyama, Ufunuo 13:16 ***"Naye akawafanya wote, wadogo kwa wakubwa na matajiri kwa maskini na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake. Hapo ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni nambari ya kibinadamu. Na nambari yake ni mia sita, sitini, sita. "***

Neno *alama* katika Kigiriki ni #5480 *charagma*, na linamaanisha *mkwaruzo* au *kuweka*, lakini pia linamaanisha *muhuri*, au *beji ya utumwa*. Wakati fulani watu wanapotoka na wanaashiria kwamba itakuwa aina fulani ya alama iliyochorwa juu ya mtu binafsi, lakini ina maana iliyo na werevu kuliko hilo tunapochukua marejeleo tofauti kutoka kwa Maandiko Matakatifu. Neno la Kiebrania ambalo tulijadili wiki iliyopita ni #8420, ambalo ni *taw*. *Taw* ni jina la herufi na linamaanisha *alama, kwa maana, sahihi*. Sasa, neno katika mzizi wake wa msingi ni *taw-waw'* ikiwa na *qames* mara mbili, #8427, na linamaanisha *kutia alama, kukwaruza* au *kutia chapa*. *Kutia chapa* pia inatupa neno lililodokezwa, *sahihi*. Ni nini basi? Tatoo? Mkwaruzo ambao unaacha kovu? Ni masikio yaliyotombolewa kama maandishi ambayo yanasema kama mtumishi




wako anataka kuendelea kukutumikia, unaweza kutomboa masikio yake kwa sindano, na atakuwa mtumishi wako daima. Ni maoni yangu kwamba Ezekieli mlango wa 9, ambao tuliangalia awali, inamaanisha kuwekwa chapa na mfumo wa Babeli upande mmoja, na kuidhinishwa na jina la Yahweh upande mwingine. *Taw* ni kama X. Wakati nilihitaji kutengeneza upya leseni yangu ya dereva, fomu ambayo ilikuja ilikuwa na X na mstari nyuma yake, ambayo ilimaanisha nahitajika kutia sahihi juu ya mstari huo. Lazima niweke jina langu nyuma ya hiyo X. Hiyo X iliwakilisha sahihi yangu.

Tunaona ukweli mkubwa ambao ninatumai hatuwezi kupitia juujuu kwa urahisi. Ezekieli 9:4:***"Yahweh akamwambia, Pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, ukatie alama*** [*taw*] ***katika vipaji vya nyuso vya watu wanaoungua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake. "*** Hivyo lazima tuwe kama Yahweh. LAZIMA TUHUZUNISHWE NA UOVU WA MFUMO HUU WA BABELI. Kwa upande mwingine, wale ambao wamechukua alama ya Babeli wako kwa mvuto ulio kinyume kwa wale ambao wanajitahidi kwa ukamilifu wa kiroho. Inahitaji kitu kinachofanya kazi kuwa na chapa na sahihi ya Yahweh. Inahitaji kitu fulani hai, basi, kuwa aliyepigwa chapa na sifa za Babeli. Ni machukizo ambayo yanafanywa na watu hawa wa Babeli, na lazima tupige kelele dhidi yake kama tunavyofanya kila siku kwenye kituo cha redio cha WMLK.

Katika Zaburi 37:37, tunaona kwamba Yahweh ataweka alama watu Wake. ***"Weka alama mtu mkamilifu, umtazame mtu mnyofu, maana kunao mwisho wenye furaha kwa mtu wa amani*** [shalom]***. Wakosaji wataangamizwa pamoja, wasio haki mwisho wao wataharibiwa. "*** Mwisho wa waovu utakatiliwa mbali. Unayo alama ya Yahweh kwa upande mmoja, imewekwa kwa mtu mkamilifu, na kwa mkono mwingine, mwisho wa safari ya wakosaji, ambao wataangamizwa milele. Ezekieli mlango wa 9 inaelezewa katika Zaburi 37:37-38.

Ni nini alama ya mnyama? Katika Ufunuo 13:16-17, tunapata nambari 600 X̅ ikitamkwa kama Chee. Kisha unapata nambari 60 ikiandikwa kama ξ, kama xsee (kama nyoka), na sita ς, kama Sigma ya mwisho katika Kigiriki kama herufi ya Kiingereza S. Tumeona miakani kwamba hili ni ufupisho wa C-h-r-i-s-t. Hiyo X ni ufupisho wa c-h-r-i-s-t, na Z na S ni Zeus. Hivyo unaweza kuisema ni C-h-r-i-s-t J-e-s-u-s (ufupisho wake). Wiki iliyopita, nilitaja kwamba katika kitabu **Biblical Numerology** kilichoandikwa na John J. Davis, anataja katika chapisho katika 1903 ambapo

**Nukuu kutoka kwa Kitabu Biblical Numerology**

"…umuhimu mkubwa wa nambari hii unaonekana tunapokumbuka kwamba ishara ya siri za upagani mkuu wa kale wa mafumbo ilikuwa SSS au 666; na kwamba leo ni kiungo cha kuunganisha kati yazo na uamsho katika kuwasiliana na pepo na theosofi ambazo zinalenga katika umoja wa dini zote katika moja.

"Ya kwanza na ya mwisho ya herufi hizi tatu ni ufupisho wa neno, Christos. Hivi kwamba, wakati tunayo x kama nyoka lenye mikunjo, imewekwa kati yazo, tunaona ishara inayofaa ya Messiah wa Shetani- mpinga-Kr-sto, uk. 145, aya ya 3, Davis, John J. Biblical Numerology (chapisho la 10), Grand Rapids: Baker Book House, 1968.

**Nambari ya Mnyama- 600, 60, 6**

Mwandishi kila wakati ametafuta kutafsiri Maandiko kwa Maandiko mengine. Kwa hiyo tunaangalia kwa Maandishi yanayohusiana kwa nambari hii.


Mia sita(600) inahusiana na vita. Angalia vifungu hivi vifuatavyo: Waamuzi 3:31, Wamuzi 18:11, Waamuzi 20:47, Kutoka 14:7, 1 Samweli 13:15, 1 Samweli 17:7, 1 Samweli 23:13, 1 Samweli 27:2, 1 Samweli 30:9, 2 Samweli 15:18, na 1 Wafalme 10:29.

Nambari mia sita, sitini, na sita ilikuwa sensa iliyochukuliwa na nabii Ezra ya vizazi vya Adonikamu (bw-na wa kupanda). Angalia pia Nehemia 7:17, ambapo kunatokea makosa katika maandishi.

Nambari mia sita, sitini, na sita pia inahusiana kwa biashara na ushuru. Angalia 1 Wafalme 10:14-15, 2 Mambo ya Nyakati 1:17, na 2 Mambo ya nyakati 9:13-14.

Nambari 60 inajumuisha nambari ya fahari ya taifa. Tafadhali geukia kwa Danieli 3:1. Hapa tunapata nambari mbili zilizounganishwa na nambari ya Mnyama, vipimo vya mnara.

Nambari 6 ni nambari ya binadamu (hakuna kiungo kisicho dhahiri katika zote Kiebrania au Kigiriki). Mtu, aliyeumbwa katika siku ya sita amepewa siku sita kila wiki za kazi, lakini nambari saba, nambari ya Yahweh ya ukamilifu wa kiroho inaonyesha Sabato. Kuhesabu huku pia kunatumika kwa mzunguko wa miaka ya sabato.




anaelezea kwamba nambari hii ni ufupisho wa neno *Christos*. Katika 1903, tayari walijua, na, kwa sababu hiyo, ikiunganishwa na C katikati, ambayo ni kama nyoka. Waliitambua katika chapisho hilo kama mpinga messiah.

Nambari hii, alama hii ya mnyama, inahusiana kwa fedha za serikali. Tunasoma katika 1 Wafalme 10:14: ***"Basi uzani wa dhahabu iliyomfikia Suleimani mwaka mmoja, ilikuwa talanta mia sita, sitini na sita, zaidi ya faida ya wachuuzi, na ya wafalme wote wa hao waliochanganyika…. "*** Ushuru ambao unakuja kutoka kote ulikuwa talanta 666 za dhahabu, ambao tuliangazia kuwa ingekuwa kama milioni $310 wakati $ 1, 000, 000 ilikuwa na thamani ya $ 1, 000, 000, sio kama ilivyo leo. ***"Mfalme Suleimani akafanya ngao mia mbili za dhahabu iliyofuliwa; kila ngao moja ilipata shekeli mia sita za dhahabu*** [hiyo ni ngao]. ***Na vigao mia tatu vya dhahabu iliyofuliwa; kila kigao kimoja kilipata mane tatu za dhahabu. Mfalme akaviweka katika nyumba ya mwitu wa Lebanoni. "*** Inahusiana kwa fedha za serikali, lakini pia inahusiana kwa dini.

Katika Danieli 3, wakati Nebukadneza aliweka sanamu ya dhahabu kwenye tambarare la Dura, nabari ilikuwa 60 na 6. Nebukadneza Mfalme alifanya sanamu ya dhahabu, na kusema "wakati mtasikia sauti ya vyombo hivi vyote- kona, filimbi, kinumbi, zeze, santuri, zomari na aina yote ya muziki (wimbo wa kitaifa, kwa maneno mengine) ukichezwa na bendi ya kitaifa- mtaanguka chini na kuabudu sanamu ya dhahabu ambayo Nebukadneza mfalme amesimamisha. Kama hutaanguka chini na kuabudu saa hiyo hiyo, utatupwa katikati ya tanuri inayowaka moto. Kwa maneno mengine, utauawa. Ikiwa hutaabudu sanamu ya Nebukadneza,

utauawa. Je, hili silo tulilokuwa tukisoma katika Ufunuo 13? Hivyo, kwa sababu hiyo, inahusiana na dini. Kama hutainama chini na kuabudu mnyama huyu, mfumo huu wa Babeli, uliofanywa na Nebukadneza, utauawa.

Kama tulivyoona awali, ulimwengu unayo nambari 600, 60, 6. Karibu kila mtu anayo 666 iliyoambatanishwa kwa jina lao, inaonekana. Katika mahali kadhaa niliyokutana nayo, Martin Luther alikuwa na 666 kama nambari ya jina lake. Upapa na baadhi ya mapapa wameonyeshwa kuwa na nambari 660 na 6. Lakini hiyo ni mnyama? Hapana, ni dhahiri silo. Adolf Hitler alikuwa na nambari 666 kwa jina lake. . Franklin Delano Roosevelt alikuwa na nambari sawa 666, kama nambari ya jina lake. Hivi maajuzi iliashiriwa kwamba Rais, au kwa sasa rais wa zamani Ronald Wilson Reagan alikuwa na nambari 666 kwa jina lake. Kila moja la majina matatu lilikuwa na herufi 6, unaona, na hivyo alikuwa na nambari 666 – Ronald Wilson Reagan. Jina la mnyama litahesabiwa wakati mfumo wa mnyama huyu utakuja kwa nguvu. Sitaelekea kuanza kutabiri jina hilo litakuwa lipi. Wakati mnyama atakuja kwa uongozi, tunajua tayari kwamba jina la kidini litatumiwa katika ibada ya mnyama huyo, na litakuwa jina la kukufuru. Jina hilo litakuwa C-h-r-i-s-t, Z-E-U-S haswa yale nakala ya Kigiriki inatuambia.

Kunalo tukio la kuvutia nilikutana nalo kuhusiana na kutawazwa kwa Charlemagne, Charles the Great kama mfalme mkuu wa kwanza wa Rumi Takatifu. Alikuwa kwenye huduma katika Saint Peter's katika Roma, na wakaabudu na kusherehekea Siri Takatifu- Katoliki, bila shakana wakamtawaza. Hilo sio picha tu ya dini ya kidunia?

Ninataka utambue kitu fulani katika 1 Mambo ya Nyakati 21:16. ***"Daudi akainua macho yake, akamwona huyo malaika wa Yahweh amesimama kati ya nchi na mbingu, naye alikuwa na upanga wazi mkononi mwake, umenyoshwa juu ya Yerusalemu*** [Yerusalemu ndiyo inafuata kupata pigo. Malaika anakuja kutoka kaskazini, na, sasa, amenyoosha upanga wake juu ya Yerusalemu]. ***Ndipo Daudi na wazee wakaanguka kifudifudi, nao wamevaa nguo za magunia. Daudi akamwambia Elohim, Je! Si mimi niliyeamuru watu wahesabiwe?*** Daudi alikuwa akisema, "*Ni mimi niliyefanya dhambi. Unaweza kulisimamisha pigo hili? Kondoo hawa hawajafanya lolote. Kwa nini umetoa pigo hili dhidi ya kondoo wako? Niue. Fungulia pigo dhidi ya nyumba yangu*"

Mstari wa 18: ***"Ndipo huyo malaika wa Yahweh akamwamuru Gadi kwamba amwambie Daudi*** [Gadi alikuwa nabii aliyesema kwa Daudi], ***ya kuwa Daudi akwee, akamwinulie Yahweh madhabahu katika kiwanja cha kupuria cha Arauna, Myebusi. "*** Basi tufikirie hili kwa muda mfupi; hapa ni Myebusi anayeishi katikati mwa Israeli, anayo shamba maarufu sana, na unaweza kuliona kutoka kwa umbali. Sakafu ya kupuria yake iko juu ya kilima na pengine Dome of the Rock ambayo bado iko kwenye jukwaa la Hekalu, Yerusalemu. Hiyo ingefanya sakafu ya kupuria nzuri. Leo imeteremka. Wapiganaji wa vita vya msalaba walikata mawe ili kuuza. Kwa wakati mmoja ilikuwa laini zaidi. Chini yake ni pango ambalo pengine wangehifadhi nafaka yao. Hivyo uwanja wa kupuria wa Arauna Myebusi pengine ulikuwa Dome of the Rock. Kama Daudi anakuja kwa Arauna, "Ni nini Myebusi anafanya akiishi katikati mwa Israeli? " Hili ni tayari miaka 400 baada ya ushindi. Jibu la pekee ambalo ninaweza kuona ni kwamba alikuwa mmoja wa watu hao walioachwa, kwa sababu alikuwa mwenye huruma kwa Ibada ya Israeli, ibada ya Yahweh. Alikuwa kama Wagibeoni. Wagibeoni walihifadhiwa na wakawa wakataji wa miti na watekaji wa maji kwa ibada ya Waisraeli. Katika maneno mengine, walikuwa wamejiwasilisha wenyewe kwa Ibada ya Kweli. Inasema, ***"Basi Daudi akakwea sawasawa na neno la Gadi, alilolinena kwa jina la Yahweh. Arauna alipogeuka, na kumwona yule malaika. "*** [Hivyo haikuwa kitu ambacho Daudi aliona, au nabii yule, lakini pia ilikuwa huyu Myebusi. ]***"Arauna akatazama, akamwona Daudi, akatoka katika kile kiwanja, akamsujudia Daudi kifudifudi hata nchi. Ndipo Daudi akamwambia Arauna, unipe mahali pa kiwanja hiki, ili kwamba nimjengee Yahweh madhabahu hapa; kwa thamani yake kamili utanipa; ili kwamba tauni izuiliwe katika watu. Arauna akamwambia Daudi, Ujitwalie, na mkuu wangu Mfalme na afanye yaliyo mema machoni pake, tazama, ng'ombe kwa sadaka za kuteketezwa, na vyombo vya kupuria kwa kuni, na ngano kwa sadaka ya unga, nazitoa; zote nazitoa. Mfalme Daudi akamwambia Arauna, La, sivyo, lakini kweli nitazinunua kwa thamani yake kamili; kwani sitamtwalia Yahweh kilicho chako, wala kutoa sadaka ya kuteketezwa isiyo na ngarama. Basi Daudi akampimia Arauna thamani ya mahali pale shekel mia sita za dhahabu kwa uzani. Kisha Daudi akamjengea Yahweh madhabahu huko akatoa***

***sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, akamwita Yahweh; naye akamwitikia kutoka mbinguni kwa moto juu ya madhabahu hiyo ya sadaka ya kuteketezwa. "***


Unaporudi nyuma kwa kifungu ambacho unasoma kuhusu katika mwisho wa 2 Samweli, ambacho ni sambamba kwa 1 Mambo ya Nyakati 21, unapata kwamba Daudi alilipia kwa ng'ombe na kuni. Alimpa Arauna Myebusi shekel 50 za fedha kwa kutoa ng'ombe na kuni kuchoma sadaka. Hivyo Arauna alitoka vizuri hapa. Alipata shekel 600 za dhahabu kwa mali yake. Malaika wa Yahweh alikuwa na uwajibikaji, kwa sababu aliambia Daudi ajenge madhabahu kwenye uwanja wa kupuria wa Arauna Myebusi. Vipi tunaweza kusema kwamba nambari 600 inahusiana kwa kiburi? Jibu ni kwamba Daudi alikuwa na kiburi sana moyoni mwake kuchukua ile mali, hivyo alitoa bei nzuri kweli kwa hicho, kama tu alivyofanya Ibrahimu ambaye alilipia shekel 400 za sarafu kwa mali ya Efroni Mhiti kumzika Sara. Pia unaweza kusema kwamba Arauna alikuwa mtu mwenye kiburi, na akakubali zile dhahabu. Katika uchambuzi wa mwisho, inasema nini? Mahali hekalu la Yahweh lilikusudiwa kusimama, mahali ambapo Yahweh alichagua, palinunuliwa na nambari ya binadamu-sita- imeambatanishwa kwake, kujaribu kuvutia kwa binadamu kwamba nambari sita bado ni yenye upungufu. 700- 7 ni nambari ya Yahweh- 700 ingekuwa nambari ya Yahweh. ***"Kisha Daudi akamjengea Yahweh madhabahu huko akatoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, akamwita Yahweh; naye akamwitikia kutoka mbinguni kwa moto juu ya madhabahu hiyo ya sadaka ya kuteketezwa. Naye Yahweh akamwamuru malaika; naye akaurudisha upanga wake alani mwake tena. "***

Walimwona huyu kiumbe asiye wa kawaida akiua watu. Haikuwa tu Daudi, lakini ilikuwa pia Arauna Myebusi, ambaye aliona huyu Malaika, na akajua kwamba hili lilikuwa kutoka kwa Yahweh. ***"Wakati huo Daudi alipoona ya kwamba Yahweh amemwitikia katika kiwanja cha Arauna, Myebusi, ndipo akawa anatoa sadaka huko. Kwa maana ile maskani ya Yahweh, aliyoifanya Musa jangwani, na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, vilikuwapo wakati huo mahali pa juu pa Gibeoni*** [imetenganishwa na sanduku, naweza kuongezea, kwa sababu Daudi alikuwa amechukua sanduku kwake mwenyewe]**.** ***Wala Daudi hakuweza kwenda mbele yake ili kumwuliza Elohim; kwa sababu aliona hofu kwa ajili ya upanga wa yule malaika wa Yahweh. "*** Malaika wa Yahweh alisimama kaskazini, kati ya Gibeoni na Yerusalemu. Wakati tupo katika Nchi takatifu, tunaweza hisia kwa karibu kwa mambo haya wakati tunaketi kwenye Mlima wa Mizeituni. Tunapoangalia kaskazini, na tunaweza kuona huko mahali pa juu pa Gibeoni. Unakumbuka kwamba malaika wa Yahweh alikuwa kati ya Gibeoni na Yerusalemu. Daudi alikuwa na hofu.

*"Pengine kama nitaenda Gibeoni, sitaweza kurudi tena kwa sababu Malaika huyo anaweza bado kuwa hapo, na labda Yahweh bado hajamaliza kunihukumia mimi kwa dhambi zangu, anasema, au angekuwa anafikiria"*

Basi kamwe tusisahau alama ya Yahweh. Tunafikiria kuihusu kila siku, kama tunasema Shema asubuhi na jioni? Tunaelewa nini Yahweh anajaribu kutuambia sisi katika Kumbukumbu la Torati 6? **"Na maneno haya, ninayokuamuru leo yatakuwa katika moyo** [hiyo ni ya ndani]**wako; nawe uwafundishe watoto wako** [hiyo ni ya ndani, neno likijitokeza na kuchukua mzizi katika mioyo ya watoto wako] **kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako** [hiyo ni ya ndani]**, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako** [hiyo ni ya ndani]**. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako** [hiyo ni ya ndani pia]**. "**Sasa ruhusu tuangalie kwa hilo kwa karibu zaidi kidogo. Tunaweza kusema kwamba ni jambo la ndani kwa Neno kuwa katika moyo wa mtu binafsi, na kumchukua huyu mtu kutoka kwa ufalme wa kinyama. Hilo linamfanya yeye kama Yahweh, kama tutafuata Agano la Yahweh. Kama tutafuata Agano la Yahweh, tutapata tabia zake. Lazima tufunze na kunena kuhusu Sheria za Yahweh. Wakati tunasema kwamba nyumba-ishara kwenye mkono, utepe katikati ya macho, miimo ya nyumba, na juu ya malango-inaweza kuwa kitu fulani cha kiroho. Pia tunaweza kuifanya kitu cha kimwili, vilevile. Inayo utafsiri mara mbili. Tumefanya hili. Tumeandika Sheria ya Yahweh kwenye miimo ya nyumba zetu. Tumeandika juu ya malango yetu, na Mwenye-nguvu Yahweh yupo hapo katika udhibiti wa mikono yetu na katika udhibiti wa akili yetu. Lazima tukumbuke, kila siku alama ya Yahweh.

Mfumo wa mnyama pia unaelezea uamsho wa Ufalme wa Rumi. Hatuwezi kupuuza nini mstari huu unasema katika Danieli 9:26: ***"Na baada ya yale majuma sitini na mawili, aliyetiwa mafuta atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu:***




***na watu wa mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika.... "*** Gharika ambayo jenerali Tito hangeweza kudhibiti: askari wa Kirumi walifurika kwenye mji na kwenye Mlima wa Hekalu. Walichoma kila kitu. Walipasua mawe yaliyojenga hekalu, mawe kutoka kwa mawe. Walipepeta majivu kupata dhahabu yote na fedha ambazo wangeweza kupata. Hivyo, kwa sababu hiyo, hili linaelezea Warumi ambao wangeharibu mji na patakatifu, na mwisho wake ingekuja kwa gharika. Kwa nini hatusemi kwamba hili ni Wababeli? Jibu, bila shaka, ni kwa sababu ya 70 saba, miaka 490. Miaka 70X7 (mizunguko ya miaka ya sabato)- miaka 490- inatupeleka hasa kwa wakati wa Yahshua. Ilikuwa kweli, Warumi ambao walimaliza mji na patakatifu mpaka Yahshua aliye Messiah atakaporudi. Baadhi ya vitabu vinatoa ishara kwamba Nero Ceasar alikuwa ambaye alibainishwa na 666, baadhi yazo Augustus Ceasar, au Julius Ceasar, au Walatini, au Warumi. Maneno haya yote yanabeba 666. Hili linaelezea mwisho wa uabudu. Ufunuo 13 ni mnyama wa pembe-mbili, wa siku za kisasa, ambaye anadaisha kwamba picha ifanywe kwa mnyama wa kwanza, kwa Ufalme wa Kirumi. Kufanya picha ambayo inaonekana kama mnyama wa kwanza, Ufalme wa Kirumi. Tunayo hali hii leo, ndugu na dada. Mataifa ya ulimwengu yameungana dhidi ya taifa moja, jinsi tu ilivyokuwa katika wakati wa Warumi. Tunao mnara mwingine wa Babeli- Umoja wa Mataifa. Tunao mfumo wa mnyama ambaye kwa kiwango fulani uliendelea katika Ulaya ya Kati, katika Brussels, katika Soko la Pamoja la Ulaya. Unabii huu unakuja kwenye mpango leo. Nafikiria tunahitaji kupata faraja katika yale tunasoma Waefeso mlango wa 6, kuanzia na mstari wa 10: ***"Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Yahweh, na katika uweza wa nguvu zake. "***Tunayo nguvu namna gani katika Imani? Tunayo nguvu namna gani katika nguvu ya uweza Wake, kumaanisha Roho Mtakatifu? Itabidi tuwe na nguvu na***"vaeni silaha zote za Yahweh, mpate kuweza kuzipinga hila [***mbinu, ujanja***] za Ibilisi. "*** Hamkumbuki ndugu na dada mlango wa tatu wa Mwanzo? ***"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Yahweh Elohim. "***Fikiria kuihusu. Shetani Ibilisi kila wakati ametawala wanyama wa ulimwengu, wote wanyama wa kimwili na serikali.

Neno la Kiebrania ambalo linamaanisha *uchi* katika 2:25, pia linatafsiriwa *werevu* au *ujanja* katika mlango wa 3:1. Katika 2:25, walikuwa uchi na uchi ni werevu au vingenevyo ni homonimu, katika Kiebrania- neno sawa linatumika.

Ni nani ambaye anaweza kusimama dhidi ya hila na ujanja wa Ibilisi? Wale ambao wanayo silaha nzima ya Yahweh, tunaambiwa kwa wazi zaidi. ***"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya nyama na damu.... "*** Hivyo hatuwezi kuwa na silaha ya chuma na ngozi. Itakuwa aina tofauti ya silaha. ***"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya nyama na damu, bali ni juu ya wakuu wa giza hili, dhidi ya uovu wa kiroho katika mahali pa juu. "*** Neno *mahali pa juu* linaleta nini kwa akili zetu, ila *bamoth* za ibada ya Baali? Sio hilo tu, lakini kwa nini tunaita Washington mji mkuu wetu (capital) wakati neno *capital* lilikuwa jina la hekalu ya

**NI WENYE NGUVU PEKEE NDIO WATASIMAMA— wale ambao wana nguvu katika tabia za Yahweh.**

**NI WENYE NGUVU PEKEE NDIO WATASIMAMA, wale ambao wana nguvu katika Roho Mtakatifu wa Yahweh**

**NI WENYE NGUVU PEKEE NDIO WATASIMAMA, ambao wamevalia vitu hivi visivyoonekana.**

Jupita? Unaweza kuthibitisha hili kwa utafiti mdogo. Kwa nini matafa ya ulimwengu yanaita miji inayoongoza, miji ya kiserikali ya mataifa ya ulimwengu, CAPITALS? Hakika linamaanisha mahali pa juu. Wakati mtu fulani anasema tunaenda kutenganisha dini na serikali, haiwezekani kufanya hilo, kwa sababu hadi kwa siku hii, wanao makasisi juu ya nyumba za mbunge, kwa mfano. Wanafuata sikukuu za kidunia za Ukristo.

Uovu wa kiroho katika mahali pa juu, wakuu wa ulimwengu wa giza hili. Inaelezea giza gani? Giza ambalo linakaa kwa dunia nzima-upofu wa kiroho ***“Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Yahweh, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni.... ”*** Hili ni kitu unachoweza kuguza na kuhisi? Hapana, ni tabia, tabia ya kiroho. Kwa hivyo, silaha za Yahweh ni kitu fulani cha kiroho, kama tu alama ya Yahweh ni kitu cha kiroho, lakini kinadhibiti mashambulizi ya Ibilisi. Inazuia mashambulizi hayo. Sio kitu unachoweza kuvalia kama unavyovalia suruali, koti au suti, lakini ni ubora wa kiroho, tabia ya kiroho. ***“Na kuvaa dirii ya haki kifuani. ”*** Hicho ni kitu kinachoonekana ambacho unaweza kuvalia? Bila shaka hapana! Ni ubora, tabia, ambayo inakuja kutoka kwa kufanya amri za Yahweh, kutuza amri Zake, Sheria na hukumu. ***“Na kufungiwa miguuni utayari tupatao kwa habari njema ya amani*** [ili kwamba hata miguu yako imelindwa na viatu, za kutimiza Utume Mkuu, kufanya kitu fulani chema kushiriki ujumbe wa wokovu na binadamu wenzetu]***Na zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani*** [vizuri, hakuna nguo halisi, lakini ni ubora, tabia. Imani ni kitu ambacho kitatuhamasisha sisi. Hakuna chochote kinaweza kuharibu imani hiyo kama tutairuhusu kuwa yenye nguvu zaidi] ***ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Chukueni chepeo ya wokovu*** [valia kitu kichwani mwako ili upanga wa Shetani usiwahi kupita], ***Na upanga wa Roho ambao ni neno la Yahweh*.... ”** Lazima tuelewe kwamba mambo haya ni yasiyoonekana, lakini ni vitu vinavyoweza kutazamwa na Yahweh, ndugu katika imani, na ulimwengu ulio nje. Tabia za washiriki wa Assemblies of Yahweh, Waabudu wa Kweli, kofia ya chuma, na upanga wa Roho, ambao ni Neno la Yahweh ambalo tunaweza kusema limeandikwa chini kwetu. Tunaweza pia kusema kwamba lazima iwe katika mioyo yetu kutuelekeza sisi. Lazima iwe akilini mwetu, kama utepe katikati ya macho yetu. Lazima iwe hapo, ikitushikilia mikono kufanya jambo sahihi, ikitudhibiti sisi.

Hilo ndilo Neno la Yahweh liliundwa kufanya. ***“Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote. ”***Na anasema *“Mimi ni balozi katika pingu, lakini ataendelea kuongea kwa ujasiri. ”*

Haijawahi kuwa inayotumika zaidi kuliko sasa kuvalia silaha zote za Yahweh au hatutaweza kusimama. Ni wenye nguvu pekee ndio watakaosimama- wale ambao wana nguvu katika tabia za Yahweh. Ni wenye nguvu pekee ndio watakaosimama-wale ambao wana nguvu katika Roho Mtakatifu wa Yahweh. Ni wenye nguvu pekee ndio watasimama, ambao wamevalia vitu hivi visivyoonekana. Lakini vinaonekana kwa Yahweh, kwa watu Wake, na walio nje. Ndugu na dada, kamwe tusisahau alama ya mnyama ni nini. Alama ya mnyama ni Shetani na tabia yake, ambayo inawekwa juu ya watu iliyochapishwa na mfumo wa Babeli, juu ya watu ambao akili yao inabakia ya binadamu na kama ya mnyama. Na Yahweh aendelee kutubariki kama tunamtumikia Yeye na kutayarisha kwa kuja mara ya pili kwa



# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

PART 4

**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Biblia bila shaka ni kitabu cha kuvutia zaidi ambacho kimewahi kuandikwa! Mara nyingi naelezea Maandiko Matakatifu kama magnum opus ya maandishi, kazi kubwa zaidi ya fasihi ambayo imewahi kuandikwa. ***"Huyu ndiye yule mwanafunzi anayeyashuhudia haya, na aliyeyaandika haya: nasi twajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli. Kuna mambo mengi aliyoyafanya Yahshua; ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa."*** (Yohana 21:24-25).

Kweli, kunazo vitabu vingi vilivyoandikwa kuhusu Biblia. Ensaiklopidia nyingi, maoni, na aina yote ya misaada kwa kusoma imeweza kuchapishwa juu ya mada ya Maandiko Matakatifu kuhusiana kwa uwepo wa Yahshua aliye Messiah. Ingawa Yohana anatuambia ukuzaji kiasi, bado kwa yote, biblia ni kitabu kikubwa zaidi na kimekuwa kitabu maarufu zaidi ambacho kiliwahi kuandikwa. Kwa kweli, mingi ya juzuu za uchambuzi ambazo zimewahi kuchapishwa kuhusu mada yoyote ni kuhusu Biblia. Kwa sababu hiyo, mwandishi wa kitabu cha Yohana, ambaye alikuwa mtume (mwanafunzi) wa Messiah, alifanya kauli ya kweli kabisa na sahihi aliposema kwamba vitabu vingi vingeweza kuandikwa. Mara nyingine tena, nakala ya Maandiko Matakatifu imethibitishwa kuwa sahihi na iliyoongozwa.

Nimekuwa najadili mada ya madarasa manne ya viumbe vilivyoumbwa ambavyo vinamhudumia Mwenye-nguvu Yahweh.

Mada tuliyoizingatia kwanza ilikuwa *makerubi*.Tulichunguza neno *cherubim* na kupata kwamba *cherubim* (kerubim, wakiwa na sauti ya *k*, au *cherubim*, wakiwa na sauti ya *ch*, kama watu wengi wanavyoitamka[ingawa kimakosa]) pia wanaelezewa kama kuwa na mwonekano ambao unajumlisha uso wa binadamu, simba, ng'ombe, tai, au nyoka. Sababu kwa nini kunao neno tofauti inayotumika hapa kati ya tai na nyoka ni kwa sababu ya maneno ya Kiebrania *nakash* (nyoka) na *nesher* (tai).

Darasa la pili la viumbe vilivyoumbwa vya Yahweh lilikuwa *maserafi*, wakipokea majina yao kutoka kwa neno la Kiebrania,kwa kuchoma. (kitenzi *seraph* kina maana ya *kuungua* katika Kiebrania.) Wao ni wanaoungua kwa sababu ya rangi yao kali, inayong'aa. Wanao mwonekano tofauti kidogo kuliko makerubi. Makerubi wanayo rangi ya yakuti, na maserafi wanayo kitu kama rangi ya kuungua sawia na shaba angavu. Maserafi wana mabawa sita wakati makerubi wanayo mabawa manne. Ingawa makerubi na maserafi wanafanana, idadi ya mabawa na rangi yao inawaweka kando.

Kumbuka, makerubi pia wanabeba kiti cha enzi cha Yahweh. Chini yao, bila shaka kuwasongeza wao, yalikuwa yale Ezekieli anaelezea katika mlango wa 1 kama magurudumu ndani ya magurudumu (baadhi ya watu wanatafsiri haya kama *gyrscope*), kuwaruhusu wao kusafiri nyuma na mbele kama umeme.

Watu wengi waaamini kwamba makerubi na maserafi ni sawa tu kama malaika, lakini tunajifunza kwamba sio hivyo. Neno la malaika ni *malachim* katika Kiebrania, au *angelos* katika Kigiriki (kutoka wapi linakuja neno la Kiingereza *angel*) Malaika ni darasa tofauti ya viumbe walioumbwa, tofauti kutoka kwa madarasa mengine matatu. Kunayo maoni potovu mazito kuhusu malaika ambayo sio ya kimaandiko. Kila wakati msimu wa Kr-smasi unapokuja, wimbo, "Sauti!Malaika Mtangazaji Imba!" unasikika. Katika Maandiko Matakatifu, malaika kamwe hawakuimba. Kuthibitisha hili ruhusu tuzingatie maandiko ya Luka 2:8 ***"Na katika nchi ile walikuwa wako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku...."*** Wimbo unaojulikana sana unasema walikuwa wameketi kwenye ardhi. Mimi binafsi najua kwamba katikati mwa msimu wa baridi, katika Desemba 25, hakuna mchungaji katika Israeli atakuwa na mifugo yake nje bila ulinzi, kwa sababu inakuwa baridi sana huko katika wakati huo wa mwaka. Nimekuwa Israeli katika msimu huo, na ni wakati unaonyesha sana. Hata kumekuwa na theluji nyingi inayoanguka karibu na wakati wa Krismasi na kugeuka kwa mwaka wa kidunia.

Yale tunasoma katia Luka lazima yalifanyika katika wakati tofauti. Nimeelezea hili katika nakala ambayo nimeandika yenye mada; **Kuzaliwa Kwa Messiah- Ni Siku Gani Alizaliwa Mwokozi?** Unaweza kuandika kwa nakala hii na kujithibitishia mwenyewe wakati wa mwaka Maandiko Matakatifu yanasema Messiah alizaliwa.

Luka anatuambia zaidi, ***"Malaika wa Yahweh akawatokea ghafla, utukufu wa Yahweh ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu. Malaika akawaambia***[kamwe hakuimba, aliongea]***, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote: maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu Mwokozi, ambaye ni Messiah aliye Mfalme***[mji wa Daudi ulikuwa Bethlehemu]***. Na hii ndiyo ishara kwenu; Mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni*** [jeshi la mbinguni likaonekana]***, wakimsifu Yahweh, na kusema*** [Sio kuimba!], ***Atukuzwe Yahweh juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu wa nia njema. Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu...."***

Wakati wachungaji wanatii amri, walipata mtoto amelala kwenye hori, SIO KATIKA BANDA. Hakuna popote kwenye Biblia tunaambiwa kwamba Yahshua alizaliwa kwenye banda. Maandiko Matakatifu yanaonyesha kwamba wazazi wapya walitumia hori- sanduku la kuwalishia wanyama- ambalo walitumia katika urasihi kama kitanda cha kulala kwa mtoto wao mchanga. Kunayo Maandiko mengi hivyo ambayo yamepotoshwa kupitia hadithi za jadi hizi za wakati wa Krismasi. Wakati Mtafutaji mwaminifu wa Kweli anasoma Maandiko Matakatifu kwa uangalifu, atapata kwamba mila zinazopendwa hazionekani kabisa kwa njia ambayo zimeonyeshwa.

Mahali pengine ambapo watu wanahitimisha kwamba malaika waliimba ni katika kitabu cha Ayubu. Katika Ayubu 38:7 tunasoma, ***"Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Elohim walipopiga kelele kwa furaha?"*** **King James Version** inasoma, "*walipoimba kwa furaha,*" lakini ruhusu tuchunguze kwa makini maandishi kuamua maana yake. Neno ni*ranan* katika nakala ya

Kiebrania, ambalo lina maana ya kupiga kelele au kelele. Walipiga kelele (au kupiga kelele) kwa furaha wakati walitambua uumbaji wenye utukufu unafunguka kwenye mtazamo ambao mwenye-nguvu Yahweh alikuwa ametarajia na sasa anauleta katika kuwepo. Walipiga kelele, "Wow" au kuweza kupiga kelele walipoona uumbaji huu mzuri ukionekana, ambao nguvu ya miujiza ya Mwenye-nguvu Yahweh ilitengeneza.

Hapa tumefuta wazo la uongo ambalo kwa kawaida linaunganishwa na malaika kupitia kufanya uchunguzi wa karibu wa Neno la Mwenye-nguvu Yahweh. Mila nyingine ninayotaka kuashiria ni kwamba malaika kwa kawaida wanaonyeshwa wakiwa na mabawa katika sanaa za kidini. Ingawa makerubi na maserafi wanaonyeshwa wakiwa na mabawa, malaika hawaonyeshwi wakiwa na mabawa. Kwa nini basi, malaika wameweza kuonyeshwa chini kupitia historia katika sanaa za kidini kama wanayo mabawa? Zamani, watu waliamini kwamba kama kitu, au kiumbe fulani kingeweza kuruka lazima kingekuwa na mabawa na kufanana na ndege wanaotumia mabawa kuruka. Tunajua sasa kwamba mabawa hayahitajiki kwa kuruka. Tangu Dr. Robert Goddard kuvumbua roketi na sayansi ya roketi kuwepo, imethibitishwa kwamba makombora yanaweza kupaa bila ya kuwa na mabawa. Nguvu zingine zinaingia kwenye mchezo ambazo zinaruhusu makombora kudumisha mwinuko na mwelekeo, kusafiri haraka na kulekezwa popote zinahitajika kwenda.

Kwa sababu hiyo, Maandiko Matakatifu yanatuambia kwamba malaika pia wanaruka, lakini hakuna popote kwenye Biblia kuonyesha kwamba malaika wana mabawa. Ndio, makerubi, na pia maserafi wanayo mabawa, lakini malaika hawana. Katika Mwanzo 18 yanaonekana maelezo ya ziara ya malaika kwa mzee Ibrahimu. Ruhusu tuisome kwetu wenyewe kuamua nini inasema.***"Yahweh akamtokea Ibrahimu karibu na mialoni ya Mamre, alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari. Akainua macho yake akaona, na tazama, WANAUME WATATU wamesimama mbele yake: naye alipowaona alipiga mbio kuwalaki...."*** Hawakuwa na mabawa kwenye migongo yao. Malaika hawa wanaonyeshwa kama watu. Na, kwa kweli ni malaika, ambalo limeweza kuthibitishwa kutoka Mwanzo 19.

Umewahi kumwona malaika? Unaweza kuwa umekuja katika mawasiliano na malaika na haukuelewa utambulisho wao wa kweli. Pengine uliangalia kwa kiumbe ukifikiria kuwa yeye ni binadamu, kama tu alivyofanya Ibrahimu. Wanaume watatu inavyoonekana, walikuja kukutana na yeye. Ibrahimu aliwaalika waingie, kwani alikuwa mtu mkarimu, na alipenda wageni. Alikimbia kukutana nao, na kuinama kwenye ardhi na kusema, "*kujeni nami na mpumzike chini ya kivuli cha mti na nitawapa kitu mle.*" Ni katika wakati wa Pasaka wakati tukio hili lilifanyika, katika msimu wa machipuko wa mwaka, na hali ya hewa ilikuwa inayokubalika sana kwa wakati huo.

Tunaweza pia kupata habari fulani zaidi juu ya mada hii kwa kugeukia Danieli 9. Tunabaini kwamba Danieli anaelewa yale yaliyoandikwa na nabii Yeremia, kwamba karibuni diaspora ya watu Wayahudi (ambao alikuwa sehemu yao) ingefikia mwisho. Alijua kwamba karibuni miaka 70 ya uhamishwaji kwa Wayahudi ingehitimishwa. Anakiri dhambi za watu wake katika kifungu hiki. Inasema katika Danieli 9:20, ***"Basi hapo nilipokuwa nikisema, na kuomba, na kuungama dhambi ya watu wangu Israeli, na kuomba dua yangu mbele za Yahweh, Elohim wangu, kwa ajili ya mlima mtakatifu wa ELohim; naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa kwa upesi, alinigusa panapo wakati wa dhabihu ya jioni...."***Kisha inaonekana maelezo ya malaika Gabrieli. Neno Gabrieli linamaanisha *shujaa wa El. Gibber* ni shujaa. Kiumbe huyu ni mmoja wa malaika maalum wa Yahweh, hata malaika mkuu pengine, ambaye anahudumu kama shujaa.

Kwa sababu hiyo, hapa ni malaika anayepaa na, kama tulivyobaini katika Mwanzo 18, wanafanya mwonekano wao kama wanadamu. Hawahitaji kuwa na mabawa kuruka, kwa sababu wanaweza, bila shaka, kama kiumbe wa roho, wanajisongeza wenyewe katika njia fulani zingine.

Sasa kwa nini ninasema kwamba hawa ni malaika watatu? Tunaweza kufikia hitimisho hili kwa sababu katika Mwanzo 19, wawili wanateremka kwenda Sodoma. Ibrahimu anawasindikiza wao kwa umbali baada ya chakula cha mchana ambacho aliwatolea, na, ninaweza kutaja, hakikuwa chakua cha mchana cha KIYAHUDI kizuri sana kilicho kosher, kwa sababu aliwapa wao maziwa (*chema*, ambacho ni kama jibini iliyopigwa), ndama (nyama), na mkate usiochachushwa, chakula ambacho Uyahudi wa kisasa hautakula, kwa sababu hawakuli nyama na maziwa pamoja. Baada ya kutayarisha bidhaa hizi za chakula pamoja, na Sara ametengeneza mkate (huo ulifanywa kwa haraka, bila shaka, mkate usio na chachu), Maandiko matakatifu yanasoma katika mwisho wa mstari

wa 8, "**NAO WAKALA**." Malaika watatu ambao walionekana kama wanaume walikula chakula ambacho Ibrahimu aliwatolea.

***"Basi wale watu wakatoka huko wakaelekea Sodoma: lakini Ibrahimu alikuwa angali akisimama mbele za Yahweh."*** (Mwanzo 18:22). Ibrahimu aliandamana nao njiani kuwaashiria njia (barabara) kuelekea Sodoma kutoka nyumbani kwake katika safu ya milima ya Yudea, iliyo karibu na katikati mwa Israeli. Ibrahimu kisha alibaki amesimama mbele ya Yahweh, lakini wanaume wengine wawili (malaika) wakaelekea Sodoma. Hawa wawili ndio kisha walikutana na Lutu na kumtoa yeye nje ya Sodoma. **"Basi wale malaika wawili wakaja Sodoma jioni; na Lutu alikuwa amekaa mlangoni pa Sodoma. Lutu akawaona akaondoka akaenda kuwalaki, akainama kifudifudi."** (Mwanzo 19:1). Unaweza kusoma kuhusu kutoroka baadaye kwa Lutu hadi Zoari (mji mdogo) na kuangamizwa kwa miji minne ya tambarare: Sodoma, Gomora, Adma na Zeboimu.

Inayoelezewa katika Mwanzo 18 ni tukio ambalo linaitwa *theophany* (udhihirisho wa Mwenye-nguvu kwa binadamu) na wanathiolojia, ambapo binadamu aliongea kwa Yeye. Hili wakati fulani ni sawia kwa yale yaliyofanyika baadaye katika maono ya Musa na Eliya wakijihusisha na Yahshua aliye Messiah katika mazungumzo juu ya Mlima wa Hermoni, wakati kugeuka sura kulifanyika. ***"Na baada ya siku sita Yahshua akawatwaa Petro na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani; akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye."*** (Mathayo 17:1-3).

Walakini, kunaye malaika mmoja wa pekee aliyewekwa kando kwa umuhimu mkubwa katika Biblia. Utamwona ameelezewa katika Waamuzi 6. Huyu ni malaika sawa wa Elohim ambaye alijidhihirisha mwenyewe baadaye katika mlango, katika Waamuzi 6:11-12a. Kifungu kinasoma: ***"Malaika wa Yahweh akaenda akaketi chini ya mwaloni uliokuwa katika Ofra, uliokuwa mali yake Yoashi, Mwabiezeri, na mwanawe Gideoni alikuwa akipepeta ngano ndani ya shinikizo, ili kuificha machoni pa Wamidiani. Malaika wa Yahweh akamtokea...."***Tafadhali pia angalia mistari 19-20.***"basi Gideoni akaingia ndani, akaanda mwana-mbuzi, na mikate isiyotiwa chachu ya efa moja ya unga, akaitia ile nyama katika kikapu, akautia mchuzi katika nyungu, akamletea hapo nje chini ya mwaloni, akampa. Naye malaika wa ELohim akamwambia, itwae nyama na mikate isiyotiwa chachu, uiweke juu ya mwamba huu, ukaumwage huu mchuzi. Akafanya hivyo."*** Malaika huyu alikuwa anashughulika na Gideoni, ambaye alimtayarisha mwana-mbuzi na mkate usiotiwa chachu na kuwasilisha kwake. Malaika kisha aliichoma kama sadaka juu ya mwamba. Tukio sawia pia linaelezewa katika Waamuzi 13, ambapo wazazi wa Samsoni, Manoa na bibi yake, walikaribiwa na malaika huyu sawa wa Elohim (*ma'alak* huyu) ***"Elohim akasikia sauti ya Manoa; naye malaika wa Elohim akamwendea yule mwanamke tena alipokuwa anaketi shambani; lakini mumewe, Manoa, hakuwapo pamoja naye."*** (Waamuzi 13:9). Hapa, kwanza alionekana kwa mwanamke (bibi yake Manoa), akimwagiza yeye asikunywe divai, au pombe kali, akimwambia kwamba angetunga mimba ya mwana ambaye angekuwa Mnadhiri tangu kutoka tumboni. Manoa hakuamini bibiye, ambaye aliripoti *theophany* hii; kwa hivyo alisema kwamba angependa kuongea kwa mtu huyu wa Elohim. Mtu huyu wa Elohim (malaika) mara nyingine alijiwasilisha mwenyewe, wakati huu kwa Manoa katika mstari wa 15. ***"Kisha Manoa akamwambia huyo malaika wa Yahweh, nakuomba tukuzuie, ili tupate kuandaa mwanambuzi kwa ajili yako."***

Baada ya Manoa kutayarisha sadaka, kisha aliomba kujua utambulisho wa malaika. ***"Manoa akamwambia huyo malaika wa Yahweh, Jina lako ni nani, ili kwamba hapo hayo maneno yako yatakapotimia nipate kukutukuza? Huyu malaika wa Yahweh akamwambia, Kwa nini wewe kuniuliza jina langu, kwa kuwa jina hilo ni la ajabu?"*** (Waamuzi 13:17-18). Huyu "Malaika wa Yahweh," kiumbe aliye na nguvu anayeelezewa kama malaika, ni Mwana wa Mwenye-nguvu Yahweh, aliye Baba. Anabeba jina la ajabu, ambalo linamaanisha, "Yahweh ni wokovu." Kuwa hakika kuangalia kwa toleo lijalo la jarida ya **The Sacred Name Broadcaster**, kama tunaendelea kwa utafiti kwenye madarasa haya manne ya viumbe Vilivyoumbwa kama utafiti huu wa kuvutia unafunguka. Andika kwa habari iliyotolewa kwa **The Sacred Name Broadcaster na Telecast** na uanze kujifunza ukweli wa kina wa kibiblia unaofunzwa na Assemblies of Yahweh. Andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel PA 19507. SNB



# Katika Kutafuta Masuke ya Kijani

*Continued from page 9.*

*nyingine. Walakini, kauli ya mamlaka pinzani, inaonekana yenye busara zaidi-kwamba ilifanywa tu hadi unga ulipokuwa laini inavyotosha, ambayo ilithibitishwa na mmoja wa 'Gizbarim' (mweka hazina) akitumbukiza mkono wake ndani yake, mchakato wa kuchunga ukiwa unaendelezwa mradi unga wowote unaambatana kwa mikono. Ingawa efa moja au omeri kumi za shayiri zilikatwa, ni omeri moja tu ya unga, au kama pinti 5.1 ya kipimo chetu ilitolewa katika Hekalu katika Paschal ya pili, ya siku ya 16 ya Nisan(makosa.) Unga uliobaki unaweza kukombolewa, na kutumiwa kwa kusudi lolote. Omeri ya unga ilichanganywa na 'logi' au karibu sana kwa robo tatu ya pinti ya mafuta, na konzi ya ubani ikiwekwa ndani yake kisha kutikiswa mbele ya [Yahweh], na konzi ikichukuliwa na kuchomwa juu ya madhabahu."*

Marejeleo yaliyodokezwa kwenye kitabu yalitolewa kwa vyanzo vya kihistoria vilivyorekodiwa katika Talmud. Ingawa, kwa kukiri, Talmud inayo makosa katika utafsiri wa kibiblia, maelezo haya ya kuvuna kwa mganda wa kwanza kukomaa yanafuata hasa njia iliyoamuriwa ya kufanya kulingana kwa maagizo ya Mwenye-nguvu Yahweh katika Neno Lake.

Umewahi kula nafaka iliyochomwa? Ni za kupendeza sana! Haswa zilizopendeza zaidi ya zote, ni ambazo unazitazama zikikomaa na kisha unazichukua wakati ambapo bado zinafika tu kwa hatua ya ukamilifu. Shayiri si tofauti. Iliyo bora kabisa ya shayiri ni masuke yaliyokomaa ya kwanza ya nafaka, yaliyochomwa, au kukaushwa, juu ya moto, pengine yanawekwa chumvi kidogo na kisha kuliwa, kama ilivyokuwa desturi katika wakati wa Ruthu.

***"Tena wakati wa chakula huyo Boazi akamwambia, Njoo hapa, ule mkate, na ulichovye tone lako katika siki yetu.Basi akaketi pamoja na wavunaji, nao wakampitishia nafaka iliyochomwa, naye akala akashiba, hata akasaza."*** Ruthu 2:14. Ni wazi, kutoka kwa kifungu hiki inaweza kueleweka kwamba Waisraeli walizingatia **nafaka iliyochomwa ya shayiri kuwa mkate kwao**. Kama miganda ya shayiri iliyokomaa inakatwa, bado kulibakia baadhi ya shayiri ambayo haikuwa imekauka na kukomaa kabisa, na hii ilichomwa na kuliwa na wafanyikazi. Hata leo, nafaka ilichomwa inaweza kununuliwa dukani. Ni ya kupendeza na ngumu, na inawezatumika kama kozi kuu ya chakula.

Uzoefu wa ukulima wakati uliopita umetuonyesha kwamba, hata katika shamba sawa, nafaka zote hazitakomaa wakati mmoja. Maeneo ya shamba moja yanaweza kukomaa kabla ya shamba nzima kukomaa vya kutosha kuvunwa. Hili ndilo kwa nini Mwenye-nguvu Yahweh amefanya amri kwamba ni nafaka pekee iliyokomaa kabisa inapaswa kukatwa kwa mganda wa kutikiswa.

Sasa tumethibitisha kabisa kwamba, kupitia kwa miaka Assemblies of Yahweh imetunza Pasaka na Sikukuu ya Mikate isiyotiwa chachu sahihi. Tumefanya hivyo kwa kutumia nyenzo hasa zilizoandikwa na hao wakosoaji ambao wangetafuta kuthibitisha tofauti. Kunayo njia moja tu iliyobakia kwa kikundi cha watu ambao wanaweza kuwa, katika siku zilizopita, wamefuata makosa, na hilo ni kutunza Pasaka ya pili.

Mwenye-nguvu Yahweh amekuwa mwenye huruma kwamba alifanya utoaji kwa Pasaka ya pili. Tafadhali angalia Hesabu mlango wa 9. Wale ambao wametiwa unajisi kwa **maiti ya mwili wa mtu** (mafundisho ya uongo yanayoongoza kwa dhambi) wanaweza kuamini kwa huruma ya Yahweh na kutunza Pasaka katika siku ya 14 ya mwezi wa pili wa kimaandiko. Kisha watakubaliwa na Yahweh, kama tu, sisi tuliyoitunza Pasaka sahihi. Lakini lazima warudi kwa wakati sahihi kwa kutunza mabaki ya siku takatifu mwaka huu, au ibada yao itakatiliwa na Mwenye-nguvu Yahweh.

Kila mwaka Assemblies of Yahweh inatuma wawakilishi hadi Israel. Wanakagua nafaka kuamua upi ni mwezi mpya sahihi wa masuke ya kijani (Abib). Unaweza kuwa hakika kwamba kama utafuata Assemblies of Yahweh kila wakati utakuwa katika mafundisho safi. Hatuwezi sema sawa kwa makundi mengine ambao wanapeperushwa huku na huku na kila upepo wa mafundisho (Waefeso 4:13-14)- kawaida wakitumia ujanja wao wa mikono, au hila kuiba washiriki kutoka kwa Assemblies of Yahweh. Jihadharini na bandia! Kunao tu Mwili mmoja wa kweli wa Waabudu wa Kweli- Assemblies of Yahweh.

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

PERIODICAL
Reading, PA

# The Sacred Scriptures, *Bethel Edition*


***"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndilo kweli."***

(YOHANA 17:17)

*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndilo kweli.*

***The Sacred Scriptures, Bethel Edition****, Inapatikana katika matoleo ya ngozi, vinyl, na ya jalada ngumu.*

*Ili kupata nakala yako ya tafsiri hii bora, andika kwa maelezo ya sasa ya bei. Au upige (717) 933-4518*




**Sasa ikipatikana kwenye Kindle**

www.assembliesofyahweh.com